# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI

## KIKAO CHA NANE

**09 FEBRUARI, 2023**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

______________________

## MKUTANO WA KUMI

## KIKAO CHA NANE – TAREHE 09 FEBRUARI, 2023

**I. DUA:**

**II. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:**

**III. MASWALI YA KAWAIDA:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**122. MHESHIMIWA FRANCIS LEONARD MTEGA (MBARALI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itapeleka Vifaa Tiba katika Hospitali ya Wilaya ya Mbarali.

**WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

**123. MHESHIMIWA GEOFREY IDELPHONCE MWAMBE (MASASI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, lini Serikali itauboresha Uwanja wa Mpira wa Boma - Masasi kwa kiwango kinachofaa kukuza na kuendeleza vipaji vya Vijana wa Masasi.

**WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

**124. MHESHIMIWA FELISTA DEOGRATIUS NJAU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuainisha nchi zenye fursa za biashara na uwekezaji ili Wananchi wazitumie kuiletea nchi yetu mapato.

**WIZARA YA MAJI:**

**125. MHESHIMIWA ANNE KILANGO MALECELA (SAME MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga mradi mpya wa maji kuliko kuendelea na ukarabati wa mradi wa Kihurio uliojengwa Mwaka 1967.

**126. MHESHIMIWA DEUS CLEMENT SANGU (KWELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itamaliza tatizo la maji kwenye Mji Mdogo wa Laela na Mpui katika Jimbo la Kwela.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**127. MHESHIMIWA DKT. JASSON SAMSON RWEIKIZA (BUKOBA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Kyatema, Kanazi, Ibwela, Katoro, Kyaka kwa kiwango cha lami.

**128. MHESHIMIWA SUBIRA KHAMIS MGALU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha za ujenzi wa kiwango cha lami kwa barabara ya Mziha – Kibindu hadi Mbwewe.

**WIZARA YA KILIMO:**

**129. MHESHIMIWA USSI SALUM PONDEZA (CHUMBUNI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni kwa nini Serikali isiongeze uzalishaji wa mafuta ya Alizeti kwa ajili ya Soko la Zanzibar na Bara kuliko kuagiza kutoka nje ya nchi.

**130. MHESHIMIWA NOAH LEMBURIS SAPUTU (ARUMERU MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, kuna mpango gani wa kutoa chakula cha bei nafuu kwa Wananchi wa Jimbo la Arumeru Magharibi kutokana na athari za ukame.

**WIZARA YA AFYA:**

**131. MHESHIMIWA ENG. STELLA MARTIN MANYANYA (NYASA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, ni lini Hospitali ya Kanda ya Kusini iliyopo Mtwara itakamilika.

**DODOMA** | **N.J. MWIHAMBI, *ndc***
**09 FEBRUARI, 2023** | **KATIBU WA BUNGE**

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA